**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS – TAMISEMI**

**Namba za Simu 0754530654**

**Mkuu wa Shule 0737951172**

**Makamu Mkuu wa Shule 0766183759**

**Matron/Patron 0762845392**

**Shule ya Sekondari KIRANDO**

**S.L.P 107 NAMANYERE**

**Tarehe 13.06.2023**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............**
**......................................................**
**S.L.P ..........................................**
**......................................................**

Yah: **MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI KIRANDO HALMASHAURI YA NKASI MKOA RUKWA MWAKA 2023**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2023 na atasoma tahasusi ya ............

Shule ya Sekondari Kirando ipo umbali wa Kilometa 63 Magharibi mwa Mji wa Namanyere Usafiri wa basi kutoka mjini Sumbawanga/Namanyere unapatikana katika kituo cha mabasi Sumbawanga na Namanyere ,Nauli ni Shilingi 10,000/= Sumbawanga – Kirando na Namanyere- Kirando ni 6,000/=.utakayetokea Mpanda utashukia stendi ya Namanyere.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe 14.08.2023 hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe 13.08.2023 Mwisho wa kuripoti ni tarehe 31.08.2023 ,kuchelewa kuripoti kutampotezea nafasi.

**2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-**

**2.1 Sare za Shule**

i. Sare ya shule hii kwa Wasichana sketi moja rangi ya blue bahari mpauko na nyeusi moja ( mshono na rangi pia urefu uzingatiwe vyote vimeambatanishwa mwishoni mwa tangazo hili.
ii. Mashati mawili meupe mikono mirefu
iii. Rangi ya Hijab (kijuba) ni nyeupe.ifunike kifua cha mwanafunzi pia iwe ndefu kufikia kifundo cha mkono akisimama
iv. Sare ya Michezo Kwa wasichana truik suit rangi ya blue
v. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi;
vi. Soksi jozi mbili nyeupe nunua
vii. Sweta rangi ya blue bahari mpauko ( siyo lazima sana kuna joto
viii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) rangi damu ya mzee drafuti ndogo mshono solo .
ix. Tai mbili zenye kufanana na sketi yaani nyeusi na blue bahari mpauko.
x. T-shirti rangi ya bluu muundo form six yenye kola nyeupe

**2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-**

i. Madaftari 07 Counter book 3q
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka;
iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika ili kumsaidia usomaji
iv. Godoro la kiwanafunzi futi 2.5
v. Mashuka Jozi 2 rangi ya pink, blanket nyepesi 1 au shuka zito kuna joto, chandarua 1 nyeupe
vi. Nguo za dharura ( kitenge na kanga 2 )
vii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe);
viii. Ndoo 2 ndogo (lita Kumi) zenye mifuniko;
ix. Kwanja 1, jembe 1, reki 1, mifagio 2 wa ndani na nje.

**ANGALIZO KUHUSU MATIBABU** : Mkatie bima ya wanafunzi aje nayo, pia hakuna special diet

### 2.3 Michango mbalimbali

**a) Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Fedha hii iwekwe kwenye akaunt ya shule**
**DEVELOPMENT KIRANDO SECONDARY SCHOOL 62001100059 NMB .**

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na

xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**


- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa).**

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Kusuka nywele
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

4. Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.




**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0754530654,0737951172,0623975951,0684829104**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0766183759,0629966020**
- **Mwandamizi Malezi 0762845392,0624700714**

**ZINGATIA HIZO NDIZO NAMBA ZILIZOKUBALIWA KWA MAWASILIANO YOYOTE HAPA SHULENI IWE KUTUMA FEDHA , ZAIDI YA HAPO JIRIDHISHE KWANZA..**


Infinix HOT 10


Infinix HOT 10


Infinix HOT 10